| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **JINA LA MTAHINIWA** | | | **NAMBARI YA MTAHINIWA** | |
| **JINA LA SHULE YAKO** | | | **NAMBARI YA SHULE** | |
| **SAHIHI YA MTAHINIWA** | | | **TAREHE** | |

# THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
# KENYA JUNIOR SCHOOL EDUCATION ASSESSMENT

**KJSEA**
**902/2**
**KISWAHILI** (*Insha na Utangulizi wa Fasihi*)
**Karatasi ya 2**
**SAMPLE PAPER**
**Januari 2025**
**Muda: Saa 1 Dakika 45**

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**
1. Andika **jina lako** na **nambari yako** ya mtihani kwenye nafasi uliyoachiwa hapo juu.
2. Andika **jina** na **nambari ya shule yako** kwenye nafasi uliyoachiwa hapo juu.
3. Tia sahihi kwenye nafasi uliyoachiwa hapo juu.
4. Andika **tarehe** ya mtihani ipasavyo.
5. Karatasi hii ina sehemu mbili; **A** na **B.**
6. Jibu maswali **yote.**
7. Andika majibu **yote** kwa nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki.
8. Majibu yote ni **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

**Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee**

| **SEHEMU** | **A** | **B** | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Zoezi I** Swali:1 | **Zoezi II** Swali: 2 | **Zoezi III** Swali:3 | **Zoezi IV** Swali:4 | **Zoezi V** Swali:5 |
| Alama ya upeo | **15** | **10** | **10** | **10** | **5** |
| Alama ya mtahiniwa | | | | | |

**Kijitabu hiki kina kurasa 12 zilizopigwa chapa.**

**Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**

*@ 2025, The Kenya National Examinations Council*

**Geuza ukurasa**

## SEHEMU A (Alama 15)

### ZOEZI I : INSHA

**Maagizo**

i. *Inapendekezwa uchukue muda wa dakika **40** katika zoezi hili.*

ii. *Andika insha yenye maneno kati ya **300 - 350** katika nafasi uliyoachiwa.*

1. Rafiki yako alikualika kusherehekea siku yake ya kuzaliwa. Kwa sababu ambayo haingeepukika, hukuhudhuria. Mwandikie barua ukimwomba msamaha.

**Geuza ukurasa**

## SEHEMU B (Alama 35)

## ZOEZI II: FASIHI SIMULIZI (Alama 10)

2. *Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu maswali*.

Hapo zamani za kale Simba na Swara walikuwa marafiki wa chanda na pete. Walitembea pamoja, walilima pamoja, waliwinda pamoja na hata kula pamoja.

Watoto wa Simba na Swara nao waliiga tabia za wazazi wao. Unajua tena mwana akibebwa hutazama kisogo cha nina. Wana hawa walikuwa mkono wazi kwa wenzao. Waliwakirimia mengi, si wanasesere wa kuchezea, si mipira ya kabumbu waliotengeneza wenyewe kwa vitambaa vikuukuu…kila kitu kizuri walichoambulia kiliwafaa wote. Ile kauli ya mkulima ni mmoja walaji ni wengi ikatimia.

Siku moja, Simba na Swara waliamua kwenda mawindoni.

"Walete wanao kwangu ili wacheze pamoja wakitusubiri tuwaletee vitoweo." Swara alimwambia Simba. Simba alikubali kwani alimwamini sana rafikiye Swara.

Walifululiza hadi kichakani kuwinda kama ilivyokuwa kawaida yao. Ghafla, Simba akajisingizia kukumbwa na jambo fulani. Alimwomba Swara aendelee kuwinda, yeye akimbie nyumbani kidogo. Swara alikubali mara moja. Simba alitimua mbio. Punde si punde alifika kwa Swara na kuwapata watoto wote wamelala. Simba aliwaamsha watoto wa Swara na kuwabembeleza kumfuata. Aliwapeleka kwenye boma lake la siri na kuwaficha huko. Aliwapa kila aina ya vitafunio nao wakafurahia sana. Simba alikuwa na mpango wa kuwala wana wa Swara mmoja mmoja hadi waishe.

Swara alipatwa na wasiwasi alipomwona mwenzake amekawia kurudi. **Alitoka shoti** na kurudi nyumbani kwake. Alipata Simba akipiga unyende huku amejishika kichwa hivi.

"Kuna nini mwenzangu?" Swara aliuliza. "Jamani hawa watoto wameingia kwenye shimo gani? Kweli mzee Fisi anaweza kuwa amewageuza kitoweo?" Alijisemea Simba bila kumwangalia Swara. Wakati wote huu Swara alikuwa anamtazama Simba kana kwamba hajamwambia lolote la kushughulisha. Swara alivuta fikra akaanza kumshuku Simba. Akajiuliza, "Kwa nini Simba aliniacha kichakani na kurudi nyumbani wakati ule?" Alianza kumfuata Simba kisiri kila mara.

Siku moja, Swara alibaki kinywa wazi alipomwona Simba akiingia katika boma lake la siri. Aliwaona watoto wao wote wakicheza kwa furaha. Hakuweza kujificha tena. Alijitokeza kwa hasira akawachukua wanawe na kurudi nao nyumbani. Simba aliona haya akashindwa kumwangalia kwa macho rafiki yake. Uzuri ni kuwa hakuwa ameanza kutekeleza unyama wake. Tangu siku hiyo, Simba na Swara wakawa maadui wakubwa. Hadithi yangu inaishia hapo.

**Geuza ukurasa**

(a) Mighani ni hadithi ambayo wahusika wake ni mashujaa. Bainisha kipera cha hadithi hii. (alama 2)

(b) Uwindaji ni moja kati ya shughuli zinazoendelezwa na jamii inayosimuliwa katika hadithi hii. Eleza shughuli nyingine **mbili** ambazo huendelezwa na jamii hii. (alama 2)

(c) Eleza sifa ya watoto wa Simba na Swara kama inavyojitokeza katika hadithi hii. (alama 1)

(d) Bainisha aina **mbili** za mandhari ambazo zimejitokeza kwenye hadithi hii. (alama 2)

(e) Kauli, 'Jamani hawa watoto wameingia katika shimo gani?' imetumiwa katika hadithi hii. Eleza mbinu **mbili** za uwasilishaji ambazo fanani angetumia kuwasilisha kauli hii. (alama 2)

(f) Eleza funzo unalopata kutoka kwa Swara. (alama 1)

**ZOEZI III: NOVELA (Alama 10)**

3. *Soma sehemu ifuatayo ya novela kisha ujibu maswali.*

Jina la Fatuma, mwanawe Bwana Makali lilikuwa na sifa si haba katika kijiji cha Mandongo kama walivyokiita wengi. Nafikiri sifa zake zilitokana na weledi wake masomoni. Ama tuseme alikuwa wembe masomoni. Fatuma alikuwa na ndoto ya kuwa mhandisi. Ndoto hii ilimsukuma kufanya kila jitihada masomoni. Alinuia kuikwamua aila yake kutoka kwenye lindi la ukata.

Shuleni, mwalimu mkuu na hata walimu wengine walimsifu Fatuma. Nidhamu pamoja na bidii yake ilikuwa ya kupigiwa mfano. Wanafunzi wenzake walimchagua kuwa kiranja mkuu wa shule. Halima, mama yake Fatuma alijikakamua kufanya kazi ya kijungu jiko ili kukidhi mahitaji ya Fatuma shuleni. Wengi walimfahamu kama Mamafua pale Mandongo. Wakati mwingine, Mamafua angeshiriki hata shughuli za ujenzi kusudi mwanawe asikose cha kutia tumboni. Hakika Mamafua alikuwa mwenye bidii ya mchwa. Fatuma naye alizidi kutia bidii masomoni.

Wakati haya yote yakitukia, Makali, babake Fatuma alikuwa amehamia katika kijiji cha Changale. Waulize wenzake nao watakwambia kugura kwake kulichochewa na utamaduni au tuseme mahitaji ya utamaduni wenyewe kwake. Mja huyu alishindwa kabisa kustahimili vijembe kwa kutoipa jamii yake mvulana wa kurithi mila za jamii yao. Fatuma naye alizidi kutia bidii masomoni. Hatimaye aliibuka mwanafunzi bora katika tathmini ya kitaifa ya mwisho wa Daraja ya Awali ya Shule za Upili.

Wanakijiji wa Mandongo walimwandalia Fatuma sherehe kubwa. Wanahabari kutoka idhaa mbalimbali walifika. Sherehe ilipambwa kwa burudani na hotuba za kumsifu na kuwahimiza wengine. Gavana wa Gatuzi la Salama alisisitiza umuhimu wa elimu ya mtoto wa kike. Wanahabari walipiga picha na kuchukua video za kila tukio la sherehe hiyo. Habari za ufanisi wa Fatuma masomoni zilisambazwa kwenye mitandao ya kijamii. Hata Makali alizipata habari hizo kutoka huko alikokuwa. Machozi ya furaha yalimtiririka.

Mashirika mbalimbali yaliahidi kufadhili masomo ya Fatuma. Aidha, shule aliyosomea Fatuma ilipigwa jeki kwa kujengewa madarasa ya kisasa. Kwa upande mwingine, juhudi za Bi Halima zilitambuliwa. Shirika la Makao Bora liliahidi kuijengea familia ya Bwana na Bi Makali nyumba ya kisasa.

(a) Kazi za fasihi huwa na malengo maalum. Eleza **dhamira** ya sehemu hii ya novela. (alama 2)

______________________________________________________________

______________________________________________________________

**Geuza ukurasa**

(b) Eleza aina **mbili** za mandhari zinazojitokeza katika sehemu hii ya novela. (alama 2)

(c) Fatuma ni mwenye matumaini maishani. Eleza sifa nyingine **mbili** za Fatuma. (alama 2)

(d) Ploti ni namna ambavyo matukio katika kazi ya fasihi yanavyojitokeza. Eleza mfuatano wa matukio katika maisha ya Bwana Makali. (alama 2)

(e) Eleza mbinu **mbili** za lugha zilizotumiwa katika sehemu hii ya novela.

(alama 2)

**ZOEZI LA IV: TAMTHILIA (Alama 10)**

4. *Soma sehemu ifuatayo ya tamthilia kisha ujibu maswali.*

**SEHEMU 2**

**Onyesho 1**

(*Ni nyumbani kwa Kubai, babuye Kaima. Kaima amemtembelea babuye kijijini baada ya kufunga shule. Kaima ni mwanafunzi wa Gredi ya 7. Begani amebeba mkoba wenye kipakatalishi. Mkononi ameshika rununu. Babu anamwona kwa mbali ila hamtambui kwa urahisi.*)

Babu: (*Akijisemea.*) Vitoto vya siku hizi vinakua upesi mno. Utadhani vimetiliwa mbolea. Ama tuseme vimepandwa kwenye udongo wenye rutuba. Lakini mbolea gani? Hii tu niliyotilia mtama wangu na haukumea hata chembe! Labda mvua iliyonyesha haikutosha. Au tuseme ni tatizo la tabianchi. Sijui mimi ...(*Kaima anakaribia aliko Babu. Babu anamtambua na kumwita kwa sauti.*) Mjukuu wangu! Mjukuu wangu! (*Kwa furaha.*)

Kaima: Naam! (*Akimkaribia.*) Shikamoo babu!

Babu: (*Huku akimkumbatia.*) Marahaba mjukuu wangu. Umefanya vyema kuja kunijulia hali. Hakika nilikuona kwa mbali nikashindwa kukutambua kwa haraka. Habari za shule?

Kaima: Njema babu. Tulifunga juzi. Tuko likizoni. Nilikuwa na hamu kubwa ya kuja kukutembelea.

Babu: Nashukuru sana kwa uamuzi wako. Hakika umekuwa mkubwa.

Kaima: (*Huku akitabasamu.*) Asante Babu. Shibe ya pale **skuli** inatunenepesha kweli. (*Akicheka.*)

Babu: (*Akimwashiria kiti akae.*) Nilikwambia mwanamume ni nguvuze. Vinginevyo utakonda kama ng’onda.

(*Simu ya Kaima inakiriza. Babu anakatiza kauli ili kumpa Kaima nafasi ya kuipokea. Kaima anaiangalia simu na kuipokea kwa uchangamfu. Anasikia sauti ya mama yake - Bi. Lucie)*

Kaima: *(Akiongezea simu sauti ili Babu asikie.) Hello! Hello! Yes Mum.* Sema, nakupata vizuri *Mum.*

Sauti: (Bi.Lucie anaongea) Ulifika kwa babu salama? Babu yukoje?

Kaima: Naam *Mum.* Nilifika salama ingawaje barabara mbovu huku kijijini zilinicheleweshа kufika kwa wakati. Inavyoonekana nitakesha huku leo kinyume na matarajio yangu. Kipakatalishi changu nacho kinakaribia kuzimika. Zoezi tulilopewa na mwalimu, sioni nikilifanyia utafiti wa mtandaoni leo.

**Geuza ukurasa**

Sauti: (*Bi.Lucie akimkumbusha.*) Lalama zako hazikuishi, mara barabara mbaya, mara stima ... Msalimie babu na umjuze kuwa tunajitayarisha kumtembelea hivi karibuni kumjulia hali.

Kaima: Pokea salamu za mamangu. Wanapanga kuja kukutembelea hivi karibuni. Anamsubiri dadangu atoke ughaibuni juma lijalo.

Babu: (*Akitabasamu.*) Nafurahi sana kusikia kwamba nyote mko salama mjini. Nina hamu kubwa kuwapokea.

(*Babu anamkaribisha kwa chajio. Wanaonekana kukifurahia kwa pamoja.*)

(*Kwa utaratibu, taa zinazima. Giza*)

(a) Mazungumzo ni mojawapo ya sifa za tamthilia. Eleza sifa nyingine **mbili** za tamthilia ambazo zinajitokeza katika sehemu hii ya tamthilia. (alama 2)

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

(b) Mshikamano wa kifamilia ni moja kati ya masuala yaliyoshughulikiwa katika sehemu hii ya tamthilia. Fafanua masuala mengine **mawili** ambayo yameshughulikiwa katika sehemu hii ya tamthilia. (alama 4)

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

(c) Eleza umuhimu wa maelezo yaliyoandikwa kwa herufi za mlazo katika sehemu hii ya tamthilia. (alama 2)

____________________________________________________________

____________________________________________________________

(d) Neno **'skuli'** ni mfano wa mbinu ya utohozi. Eleza mbinu nyingine **mbili** za lugha zilizotumiwa katika sehemu hii ya tamthilia. (alama 2)

______________________________________________________________

______________________________________________________________

**ZOEZI V: USHAIRI (Alama 5)**

5. *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali*

Najibwaga uwanjani, ya moyoni kuyasema,
Nyote myatazameni, mnayotenda si mema,
Sitiane hatiani, endelezeni heshima,
Heshima ni kitu chema, nyie wana fahamuni.

Nyie wana fahamuni, hinunuliki heshima,
Heshima ni mhisani, pia huleta neema,
Utamlaumu nani, matendoyo kikuuma?
Heshima ni kitu chema, nyie wana fahamuni.

Mkiwa huko shuleni, tendayo au kusema,
Michezo na kote fani, wanafunzi na ulama,
Shule na pia nyumbani, heshima ni kubwa dhima,
Heshima ni kitu chema, nyie wana fahamuni.

(K. David)

(a) Eleza ujumbe wa shairi hili. (alama 2)

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

**Geuza ukurasa**

(b) Ni wahusika gani wanashauriwa katika shairi hili? (alama 1)

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

(c) Bainisha mbinu **mbili** za lugha zinazojitokeza katika ubeti wa **pili.** (alama 2)

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.**